*Mulika, Na. 42 (1), 15-32*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Mabadiliko ya Kiuimbaji ya Nyimbo za Ibada katika Kanisa Katoliki Tanzania: Uchunguzi wa Makanisa Teule

*Kassomo Athanas Mkallyah*[1]
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.2

**Ikisiri**

Makala haya yanahusu mabadiliko ya kiuimbaji ya nyimbo za ibada na athari zake katika Kanisa Katoliki, Tanzania. Makanisa mawili ya kikatoliki ya Dar es Salaam yalichunguzwa, Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu na Kanisa la Mtakatifu Paulo Mtume Ubungo-Msewe. Makanisa haya yalichaguliwa kutokana na kuwepo kwa wamisionari wageni na wazawa waliosaidia kupatikana kwa taarifa muhimu za utafiti uliofanyika. Njia zilizotumika kukusanya data ni utalii wa uwandani, mahojiano na majadiliano. Utafiti uliofanyika ulilenga kujibu maswali yafuatayo: ni mabadiliko gani ya kiuimbaji yaliyotokea katika nyimbo za ibada za kikatoliki Dar es Salaam? Ni mambo gani yaliyosababisha mabadiliko ya uimbaji wa nyimbo za ibada katika Kanisa Katoliki Dar es Salaam? Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Utendaji. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa yapo mabadiliko katika muktadha wa utunzi wa nyimbo, maudhui, lugha, na waimbaji wa nyimbo yaliyoleta uhuru wa kusali kwa Watanzania na kulijenga kanisa lao. Mabadiliko haya yalisababishwa na kupatikana kwa uhuru wa Tanzania Bara, Mtaguso wa Vatikano II, utamadunisho, biashara na kukua kwa sayansi na teknolojia Tanzania.

## 1.0 Utangulizi

Wimbo ni sanaa inayojikita katika melodia inayoambatana na utamkaji wa maneno ya lugha yanayobeba utamaduni wa kabila la watu. Sanaa ya nyimbo hubeba ujumbe na kuufikisha kwa hadhira kwa njia ya melodia inayofuata mpangilio wa mapigo maalumu ya ridhimu. Nyimbo ni moja ya kipera cha tanzu za fasihi simulizi, ambacho hughaniwa na kutongolewa kwa mdomo. Aidha, wimbo ni kipera cha ushairi katika fasihi simulizi kinachotegemea muktadha (Wamitila, 2004). Nyimbo hujibainisha katika aina kuu mbili: mosi, nyimbo za kimapokeo au kitamaduni ambazo hutungwa kwa muktadha wa jamii husika (King'ei na Kisovi, 2005); pili, nyimbo za kisasa ambazo hutungwa na kumilikiwa na msanii. Nyimbo zote hutungwa kwa kutumia melodia zinazoelezea hali za binadamu kama vile uchungu, huzuni, na furaha**.** Aidha, nyimbo za ibada za Kikristo au muziki mtakatifu hujengwa na melodia za sauti za binadamu na maneno yake aghalabu

[1] **Baruapepe:** kassomomkallyah67@gmail.com

hutoka katika Biblia, hasa kitabu cha Zaburi au Tenzi za Rohoni (Sanga, 2006). Pia, maneno ya nyimbo hizo yanaweza kutoka kwenye "tafakuri ya mababa wa kiroho hasa Baba Mtakatifu, maaskofu na mapadre." (Mahojiano na Kadinali Pengo, tarehe 20/3/2020). Nyimbo hizi zina nafasi kubwa na muhimu katika kuongoza ibada, kusali, na kuwaunganisha watu/waumini katika kumtukuza Mungu wao.

Katika Kanisa Katoliki, uimbaji ni ibada na ibada ni uimbaji kama Papa Augustino anavyosisitiza kuwa mtu anayeimba vizuri wakati wa ibada husali mara mbili (Kilaini, 2007). Lakini ni vigumu mtu kuimba vizuri wakati wimbo ni mbaya, hivyo ili aimbe vizuri ni lazima wimbo uwe mzuri. Dhana ya uzuri au ubaya ni tata. Katika sanaa, uzuri hujitokeza kama thamani au sifa ya juu ya mpangilio wa mfumo ambao unawasilisha na kutambulisha ufundi wa muundaji wa kazi ya kisanaa inayohusika (Wamitila, 2004). Aidha, ubaya ni udhalilifu wa mpangilio wa mfumo wa kazi ya kisanaa inayowasilisha au kutambulisha uwi kwa muundaji au mtendaji au hadhira ya kazi ya kisanaa inayohusika. Dhana ya uzuri na ubaya hutawaliwa zaidi na desturi, mila, kaida, na tamaduni za jamii husika (Blackwell, 2004). Kutokana na dhana hizo za uzuri au ubaya, mambo ya kuhoji ni: Vigezo gani vinavyofanya wimbo uwe mzuri au mbaya? Je, ni melodia au maneno yaliyotumika? Je, ni ridhimu au mdundo wake? Je, ni wimbo mzuri au mbaya kwa nani? Je, ni kwa viongozi wa kanisa, waimbaji wenyewe, waumini, wasikilizaji au Mungu anayeabudiwa katika ibada? Pengine ni vema kanisa likabainisha vigezo vya wimbo mzuri au mbaya katika ibada. Ili kujibu maswali haya, mawazo ya watafitiwa mbalimbali yalitumika. Kwa mujibu wa Mwadhama Kadinali Pengo, aliyekuwa Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, "wimbo wowote unaotumika katika ibada ni mzuri endapo tu maneno yake yametoka katika Biblia, hasa Zaburi, au tafakuri za mababa watakatifu" (Mahojiano, tarehe 20/3/2020).

Naye DeBellis (1995) anasema, "Ikiwa wimbo ni mzuri, kwa kawaida, hadhira hushiriki katika utendaji wake; na kama haukuibua hisia, basi hadhira hujitenga nao" (uk. 56). Hoja hii inachagizwa zaidi na utamaduni wa hadhira inayosikiliza wimbo. Ikiwa wimbo huo umechota mirindimo, melodia au ghani na maneno kutoka kwenye utamaduni wa hadhira husika, basi wimbo huo ni mzuri kwa hadhira hiyo kwa sababu hadhira hiyo hupata hisia kutokana na wimbo huo (Kivy, 2001); na endapo wimbo huo hauna mirindimo, melodia au ghani na maneno yanayotoka katika tamaduni za hadhira hiyo, basi wimbo huo ni mbaya kwa sababu hauwezi kuivutia hadhira hiyo. Kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa na watalamu hawa, wimbo mzuri wa ibada ni ule wenye mirindimo, melodia au ghani kutoka utamaduni wa hadhira husika unaotumika katika ibada ili kumtukuza Mungu. Pia, wimbo mzuri wa ibada huchukua maneno kutoka kwenye Biblia au tafakuri za mababa watakatifu, na unapoimbwa huibua hisia, hushirikisha waumini, viongozi wa kanisa na watu wote katika ibada.

Kwa kipindi kirefu ibada za kikatoliki zilitawaliwa na uimbaji wa nyimbo. Nyimbo hizi zilitegemea zaidi kiongozi aliyeongoza ibada, hasa padre au katekista. Kiongozi huyu ndiye aliyechagua na kuanzisha wimbo uliopokelewa na waumini wote. Uimbaji huu ulishirikisha waumini wote wakati wa ibada, na ulijulikana kama uimbaji wa "pamoja au wa ushirikishwaji" (Wagner, 2016:115). Aidha, upo uimbaji unaojumuisha watu wachache au kikundi cha waumini kiitwacho kwaya ambacho huimba kwa niaba ya kanisa zima. Kikundi hiki huwaongoza waumini kusali kwa kufuatisha kuimba kwa pamoja "nyimbo zinazojulikana na wote ili kumtukuza Mungu wakati wa ibada" (Mangi, 2015:14).

Tangu Kanisa Katoliki lianzishwe nchini Tanzania, kwenye karne ya 18, nyimbo za ibada zilitumika katika ibada za ndoa, ubatizo, komunyo, Krismasi, Pasaka, na ibada za kawaida (Baur, 2005). Aidha, nyimbo hizi "zimebadilika kwa kiasi kikubwa" tangu dini ilipoanzishwa hadi sasa (Sanga, 2010:149). Hivyo, makala haya yanaeleza mabadiliko ya kiuimbaji ya nyimbo za ibada na athari zilizotokea tangu Kanisa Katoliki lilipoanzishwa nchini Tanzania.

## 2.0 Nadharia ya Utendaji katika Nyimbo za Ibada za Kikristo

Makala haya yametumia Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Schwartz L. mwaka 1945 na kutumiwa na wataalamu mabalimbali akiwemo Gelfand na Schwartz (Schwartz, 2010). Nadharia hii inajikita katika vipengele vinavyolizunguka tukio la utendaji hasa nyimbo, waimbaji, wapiga ala na hadhira. Nadharia ya Utendaji inaamini kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya nyimbo na uimbaji, waimbaji na nyimbo, na ala na waimbaji. Uhusiano huu huathiri mambo yanayohusisha tukio la kisanaa hasa uimbaji, uchezaji, eneo la kuimbia, usimamaji na ukaaji wakati wa kuimba. Pia, huathiri lugha iliyotumika katika nyimbo na ala zilizotumika kusindikiza uimbaji. Aidha, haiba ya mwimbaji hususani uvaaji wa maleba, mitindo ya nywele iliyotumika na muonekano wa mwimbaji kwa ujumla nao huathiriwa. Kwa ujumla, hali ya utendaji katika nadharia hii huathiriwa na mambo makuu matatu; "mwimbaji, mtazamaji na eneo halisi au lisilo halisi linalotumika kuimbia au kusaidia utendaji wa kisanaa" (Mulokozi, 1996:15). Katika nadharia hii, mwimbaji ndiye mtendaji mkuu kwa sababu ndiye mwandaaji wa nyimbo, mwimbaji, na mchaguzi wa sehemu ya kuimbia nyimbo hizo.

Hivyo, kwa kutumia nadharia hii, mtafiti aliweza kuchunguza nyimbo za ibada katika Kanisa Katoliki, Dar es Salaam, waimbaji wa nyimbo hizo, uimbaji wao, eneo lililotumika kuimbia nyimbo, ala za muziki, uvaaji pamoja na uchezaji uliotumika wakati wa kuimba nyimbo hizo. Pia, mtafiti aliweza kuchunguza muktadha wa utunzi, maudhui, melodia na lugha iliyotumika kuimbia nyimbo hizo. Vilevile, mtafiti alichunguza mambo yaliyosababisha nyimbo hizo ziimbwe kwa lugha hizo. Aidha, nadharia hii ilisaidia kuchunguza mabadiliko yaliyojitokeza kwa waimbaji, waumini na Kanisa Katoliki kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, nadharia ya Utendaji ilimpa mtafiti nafasi ya kushiriki katika kuimba, kuchunguza na kusawiri dhamira ya nyimbo za ibada na matukio yaliyofanywa na wanakwaya, yakihusianishwa na jamii husika. Nadharia hii ilisaidia kuchunguza jinsi mwanakwaya alivyoishi, ushiriki wake katika nyimbo za ibada za kikatoliki na uhalisia wake kijamii kwa kupitia uimbaji wake. Aidha, data zilizokusanywa katika utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Utendaji ikijiegemeza kwenye misingi ya nadharia.

**3.0 Njia za Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu ulitumia njia ya mahojiano, ushiriki na majadiliano katika kukusanya data. Utafiti huu ulifanyika katika makanisa mawili ya kikatoliki, Kanisa Kuu la Kiaskofu la Mtakatifu Yosefu na Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo Mtume Ubungo-Msewe, yote ya jijini Dar es Salaam. Kanisa Kuu la Kiaskofu la Mtakatifu Yosefu lilichaguliwa kutokana na upatikanaji wa vyanzo mbalimbali vya historia ya Kanisa Katoliki nchini Tanzania kama vile, nyimbo za ibada tangu kipindi cha uenezaji wa dini ya Kikristo hadi sasa.

Vilevile, viongozi waanzilishi wa Kanisa Katoliki Tanzania na viongozi wengine mashuhuri katika kanisa hili walipitia hapa; kwa hiyo, habari zao za uongozi wao katika ibada kwa wakati huo zilisaidia kuonesha jinsi uimbaji wa nyimbo za ibada ulivyokuwa kwa kipindi hicho. Pia, kuwepo kwa kwaya ya Mtakatifu Yosefu, ambayo imedumu kwa kipindi kirefu na kupitia mabadiliko mbalimbali ya kiuimbaji katika Kanisa Katoliki nchini, kulisababisha kuchaguliwa kwa Kanisa Kuu la Kiaskofu. Aidha, kanisa hili lilikuwa muhimu kwa upatikanaji wa sampuli mbalimbali za nyimbo zilizoimbwa kwa vipindi tofauti tangu ukristo ulivyoingia Dar es Salaam. Pia, vyombo vya habari vya Kanisa Katoliki, Redio Tumaini, Televisheni Tumaini na gazeti la Tumaini, vilivyo na taarifa nyingi za uimbaji wa nyimbo za ibada za Kanisa Katoliki vilipatikana hapa.

Pia, uchaguzi wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo Mtume, Ubungo-Msewe ulitokana na kuwapo kwa wanakwaya waliyoimba kwa muda mrefu. Pia, kuwepo kwa mapadre wa kigeni wa Shirika la Konsolata kulisaidia kuona jinsi nyimbo zilivyoimbwa kwenye ibada zilizoongozwa na mapadre wa kigeni. Vilevile, kuwepo kwa wataalamu wakongwe wa muziki wa kanisa waliotumikia Kanisa Katoliki kwa kipindi kirefu kama Mwalimu Dionisius Mbilinyi, Mwalimu Sabinus Komba na wengine wengi ulisaidia kupata taarifa mbalimbali za uimbaji wa kikatoliki nchini Tanzania.

Vilevile, kuwepo kwa kwaya ya Mtakatifu Paulo Mtume na kwaya ya Bikira Maria Konsolata ambazo zimehudumu kwa muda mrefu katika kanisa hili, kulitoa mchango mkubwa wa nyimbo za ibada za kikatoliki kwa utafiti huu. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa ambapo kwaya mbili za Mtakatifu Yosefu kutoka kanisa kuu la Kiaskofu la Mtakatifu Yosefu na kwaya

ya Mtakatifu Paulo Mtume kutoka Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo Mtume zilichunguzwa. Pia, mtafiti alichagua sampuli kutoka kwenye nyimbo zilizokusanywa kwenye utafiti na kuzichambua kulingana na jinsi zilivyokidhi malengo ya utafiti huu. Aidha, maswali yafuatayo yaliongoza utafiti huu: Je, ni mambo gani yaliyosababisha mabadiliko ya kiuimbaji ya nyimbo za ibada za kikatoliki jijini Dar es Salaam? Je, ni mabadiliko gani ya kiutendaji yaliyotokea katika nyimbo za ibada za kikatoliki jijini Dar es Salaam? Ni athari gani zilizosababishwa na mabadiliko hayo? Katika kujibu maswali haya, makala yalitumia Nadharia ya Utendaji kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu.

## 4.0 Nyimbo za Ibada katika Kanisa Katoliki Tanzania

Historia ya nyimbo za ibada katika Kanisa Katoliki nchini Tanzania ilianza kipindi cha ujio wa Wamisionari walioleta dini ya Kikristo mnamo karne ya 18. Wamisionari hawa walianzia Zanzibar na kuendelea Bagamoyo, "Pugu, na baadaye kujenga Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu pembezoni mwa Bahari ya Hindi" ambalo ndiyo makao makuu ya jimbo kuu la Dar es Salaam hadi leo (Baur, 2005:15). Watanzania kwa muda mrefu walikuwa na dini zao za asili zilizojikita katika imani iliyowaongoza kuishi kwa umoja, upendo, na mshikamano. Dini hizi ziliwapa nafasi ya kumwabudu Mungu wamtakaye kwa kutumia nyimbo zao za asili (Mkallyah, 2005). Wamisionari walipokuja walianzisha dini ya Kikristo iliyojipambanua kwa madhehebu mbalimbali yakiwamo Anglikani, Lutherani, Moravian, Pentekoste, Sabato, na Romani Katoliki.

Wamisionari hawakuruhusu nyimbo za kitamaduni zilizoimbwa na Watanzania katika ibada zao za asili, kutumika katika ibada za Kikristo. Nyimbo za kitamaduni waliziita za kipagani zilizojaa dhambi, hivyo, hazikutakiwa kutumika katika ibada za Kikristo. Aidha, Mkristo yeyote "hakuruhusiwa kuimba nyimbo za Kiafrika nje au ndani ya kanisa" (Collins, 2004:119). Mkristo yeyote aliyeimba nyimbo hizo alikuwa ametenda dhambi, hivyo alifukuzwa au alitengwa na kanisa mpaka afanye kitubio (Kidula, 2008). Aidha, nyimbo za kigeni zilizoletwa na Wamisionari ndizo zilizotumika katika ibada za Kikristo.

Kwa kipindi kirefu, katika ibada za Kikatoliki, nyimbo nyingi za kigeni ziliimbwa kwa lugha ya Kilatini ingawa lugha ya Kiingereza ndio ilikuwa ikitumika katika ibada. Watanzania walilazimishwa kufuata imani ya Kikristo na kutumia nyimbo za kigeni (Kidula, 2013). Mabadiliko haya yaliwafanya Watanzania kuwa wageni wa kiutamaduni katika nchi yao. Aidha, lugha hizi za kigeni zilizotumika katika nyimbo, ibada na shughuli za wamisionari, ziliwagawa na kuwatenga Watanzania katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni la Watanzania waliopokea ukristo na ambao walijitahidi kutumia lugha za kigeni za wamisionari. Watanzania hawa walitumika pia kama wasaidizi au watumishi wa wakoloni (Odwar, 2005). Kundi hili lilionekana kuwa linakubaliwa na Mungu, na kwamba wao watafika mbinguni. Kundi la pili ni la wapagani waliokataa imani ya Kikristo. Kundi hili

lilijumuisha watu waliotumia lugha za asili. Watanzania hawa walionekana kuwa wenye dhambi, watu ambao walistahili kwenda Jehanamu kwenye moto wa milele (Lihamba, 2004; Mkallyah, 2005). Hali hii iliwafanya Watanzania kuwa wanyonge nchini mwao kwa kuacha utamaduni wao.

Kama ilivyoelezwa, nyimbo nyingi katika ibada za Kikatoliki zilikuwa zikiimbwa kwa lugha ya Kilatini, hali hii ilisababisha kuenea zaidi kwa lugha hiyo ulimwenguni kote. Hali hii ilitokana na makao makuu ya kiongozi wa Kanisa Katoliki kuwa Italia-Roma, ambako lugha kuu inayotumika huko ni Kilatini. Padre Malema alipohojiwa kuhusu kutumika kwa lugha ya Kilatini katika Kanisa Katoliki alisema "mapokeo ya kanisa yanatuambia kuwa Kilatini ndiyo lugha iliyotumiwa na Baba Mtakatifu, yaani Papa huko Italia, hivyo, lugha hiyo ndiyo iliyopitishwa kuwa lugha ya Kanisa Katoliki ulimwenguni" (Mahojiano na Padre Malema, 20/2/2019). Hivyo, ibada na nyimbo zote zilizotumika katika kanisani katoliki ziliimbwa kwa Kilatini. Baadhi ya nyimbo hizo ni "Bwana utuhurumie, yaani *Kriye*, Utukufu-*Glory*, Mtakatifu-*Sactus*, Baba yetu-*Pater noster* na Mwanakondoo-*Agnus Dei*" (Mahojiano na Padre Malema, 20/2/2019). Kwa mfano, wimbo wa Mwanakondoo-*Agnus Dei* ulioimbwa kwa Kilatini ulikuwa na maneno yafuatayo:

***Agnus Dei***
*Agnus Dei, qui tollis peccata mundi: misere nobis.*
*Agnus Dei, qui tollis peccata mundi: misere nobis.*
*Agnus Dei, qui tollis peccata mundi: dona nobis pacem.*

**Tafsiri.**
**Mwanakondoo wa Mungu**
Mwanakondoo wa Mungu uondoaye dhambi za dunia utuhurumie.
Mwanakondoo wa Mungu uondoaye dhambi za dunia utuhurumie.
Mwanakondoo wa Mungu uondoaye dhambi za dunia utujalie amani.

Kutokana na wimbo huu kuimbwa kwa Kilatini, ilikuwa vigumu kwa waumini wengi kuimba na kufahamu maana ya wimbo huu. Hivyo, utumiaji wa nyimbo za kigeni, hasa Kilatini, ulileta mabadiliko makubwa katika ibada za Kikatoliki. Awali, nyimbo hizi ziliimbwa na mtu mmoja tu aliyefahamu vizuri lugha hiyo na nyimbo hizo, hasa kiongozi wa kanisa, yaani padre au katekista. Kadiri kanisa lilivyoenea, kulijitokeza watu wachache waliojifunza kidogo Kilatini. Watu hao ndiyo walikuwa waliimba kwa niaba ya kanisa zima. Hali hii ilieneza sana utamaduni wa kigeni hasa wa Kilatini katika kanisa na kudidimiza utamaduni wa Mtanzania. Hata hivyo, uimbaji huu ulikuwa wa kukariri tu maneno pasipo kujua lugha hiyo inavyotumika. Vilevile, waimbaji wa nyimbo hizi waliheshimiwa kama watumishi wasaidizi wa kanisa. Kwa upande mwingine, "nyimbo za kigeni zilichangia Ukristo kutokuenea kwa haraka Afrika" kwa kuwa ziliwatenga waumini wa Kiafrika na Mungu wao na hivyo, kuwafanya wawe wasikilizaji tu (Adeola, 2020:91).

Baada ya Wamisionari kugundua kuwa uenezaji wa dini ya Kikristo kwa Waafrika haukwenda haraka, mabadiliko mengine yalianza kutokea. Melodia za Kiafrika zilizokuwa zimekataliwa kanisani na Wamisionari kuwa "ni za kipagani na hazifai kutumika katika ibada za Kikristo, zilianza kutumika" (Emielu, 2010:293). Melodia hizi ziliwekewa maneno ya lugha za kigeni. Kwa mfano, misa Luba Lunda ya Kongo iliimbwa kwa melodia ya Kikongo lakini lugha iliyotumika ni ya Kilatini. Pia, misa iliyojulikana kwa jina la Baba yetu iliyoimbwa kwa melodia ya Kingoni ilitumia lugha mchanganyiko ya Kiswahili na Kingoni (Mbunga, 1959). Ubunifu wa utumiaji wa melodia asili katika ibada za Kikatoliki uliwatambulisha Waafrika hususani Watanzania kwa utamaduni wao na kuleta mabadiliko makubwa yaliyowafanya Waafrika wengi kuanza kushiriki katika ibada kwa kuimba melodia walizotumia katika jamii, japo ziliwekewa maneno ya lugha ya kigeni (Yung, 2019).

**5.0 Mabadiliko ya Kiuimbaji katika Kanisa Katoliki Dar es Salaam**

Mabadiliko katika kazi hii ni hatua ya "kutoka hali moja kwenda hali nyingine tofauti na ile ya awali" (TUKI, 2004). Mabadiliko hutokea katika miktadha mbalimbali katika jamii yakihusisha kitu au mtu mmoja, kundi la watu, jamii au taasisi fulani. Kutokana na data zilizokusanywa, ilibainika kuwa nyimbo zilizoimbwa na wamisionari walioanzisha Kanisa Katoliki Tanzania zilikuwa tofauti na nyimbo zinazoimbwa kipindi hiki hasa katika kipengele cha lugha. "Baada ya uhuru wa Tanganyika, nyimbo chache za ibada zilianza kutafsiriwa na kuimbwa kwa Kiswahili kidogo kidogo kwa kuwa hakikueleweka zaidi" (Mahojiano na Mwalimu Mbilinyi, 17/3/2019). Hivyo, uimbaji wa nyimbo kwa Kiingereza na Kilatini kwa kuchanganya na Kiswahili ulianza kutumika taratibu.

Kwa upande mwingine, data zilionesha kuwa baada tu ya Azimio la Arusha kuanzishwa mwaka 1967, mkazo mkubwa ulikuwa matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote za jamii. Lugha ya Kiswahili ilichochea pia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na Elimu ya Watu Wazima kwenye miaka ya 1970 (Lihamba, 2004). Kipindi hiki nyimbo zote na misa zilizotumika zilitafsiriwa na kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili, jambo lililowafanya Watanzania wengi, ndani na hata nje ya kanisa, waliosikiliza nyimbo hizo kuelewa ujumbe. Pia, vitabu vya nyimbo za ibada kama *Tumsifu Mungu*, *Chuo Kidogo cha Sala*, na *Nyimbo Zetu* zilizotungwa na Kanisa Katoliki miaka ya 1970 na kuendelea vilitumia lugha ya Kiswahili. Wimbo wa "Utukuzwe" uliorekodiwa na Shirikisho la Kwaya Katoliki Dar es Salaam, SHIKWAKADA (hivi sasa UKWAKADA), wakati wa ujio wa Baba Mtakatifu, Papa Yohane Paulo wa Pili, nchini Tanzania mwaka 1990, wenye kiitikio cha maneno yafuatayo ni mojawapo ya nyimbo zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili.

> Utukuzwe ewe baba Mungu utukuzwe, aleluya aa x2
> Utukuzwe, utukuzwe baba muumba ulimwengu, aleluya aa x2
> Tumepokea mkate chakula cha uzima, aleluya aa
> Tumepokea divai ni tunda la mzabibu, aleluya aa.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika wimbo huu yaliwahamasisha waumini kuimba wimbo huu wakati wa ibada. Hali hii iliwaongezea Watanzania uhuru na kujiamini zaidi katika ibada, shughuli zao na kanisa kwa ujumla. Aidha, kwa kutumia lugha ya Kiswahili, nyimbo za ibada zilipata nafasi ndani na nje ya ibada. Kwa mfano, mtafiti alishuhudia wimbo wa "Utukuzwe" uliokuwa ukiimbwa wakati wa ibada, sehemu ya sadaka, ukiimbwa kwenye ukumbi wa sherehe ya harusi na ubatizo iliyofanyika Ubungo tarehe 9/1/2021. Mama Kamungu, mwimbaji wa kwaya ya Mtakatifu Paulo Mtume ya Ubungo-Msewe, alipohojiwa juu ya matumizi ya nyimbo za ibada, alisema, "nyimbo za ibada zilianza kuimbwa nje ya ibada baada tu ya kuanza kutumia Kiswahili, lugha ya watu wengi" (Mahojiano na Mama Kamungu, 22/5/2021). Hali hii iliongeza matumizi ya nyimbo hizi kutoka nyimbo za ibada na kuwa nyimbo za shughuli za kijamii kama vile, sherehe za harusi, ubatizo, komunyo na hata sherehe za kiasili (taz. Chitanda, 2002). Hivyo, nyimbo hizi zilieleweka kwa watu wengi.

Pamoja na wimbo huu kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili, ilibainika kuwa melodia yake ilikuwa ya Kingoni. Aidha, nyimbo nyingi zilizochunguzwa zilikuwa za kiasili. Miongoni mwa nyimbo hizo ni kama vile, "Bethlehemu katika Mji wa Yuda" (Kisukuma), "Twendeni kwa Bwana" (Kihehe), n.k. Matumizi ya melodia za kiasili katika nyimbo za ibada kama vile ilivyokuwa katika Misa Luba Lunda 1958 ya Kongo, yaliwavuta watu wengi hasa Waafrika kujiunga na kanisa. Melodia hizi ziliambatana na ala za kiasili kama filimbi, kayamba, na ngoma za asili zikichanganywa na kinanda. Hali hii ilileta ladha na vionjo vipya kanisani. Aidha, matumizi ya ala za asili na melodia hizi yaliondoa mawazo hasi yaliyojengwa na wamisionari kuwa ni dhambi, na hivyo "sasa zilitumika kanisani kwa utukufu wa Mungu" (Emielu, 2010:293). Kwa upande mwingine, matumizi ya melodia ya Kingoni katika wimbo "Utukuzwe" ikiwekewa maneno ya Kiswahili, ilitoa uhuru mkubwa kwa Watanzania kushiriki ibada kwa kujiamini na hivyo, kumsifu Mungu wao.

Mabadiliko mengine yaliyoonekana katika nyimbo za ibada za Kikatoliki ni matumizi ya lugha za mitaani. Nadharia ya Utendaji inaeleza kuwa ili utendaji uwe kamili ni muhimu uendane na wakati unaoruhusu tendo hilo kutendeka. Kwaya zilizotafitiwa zilionesha kuwavutia wateja kwa kuwa ziliimba nyimbo zilizotumia lugha za mitaani zilizoendana na wakati na jamii kwa ujumla. Miongoni mwa nyimbo zilizotumia lugha za mitaani ni "Yesu Amechakachuliwa", "Mchanganyo", "Kidole Juu", na "Mshipi wa Yesu". Lugha za mitaani zinafuata wakati, matumizi na mahitaji ya jamii husika. Kwa mfano, mtafiti alishuhudia wimbo wa "Mchanganyo" ukiimbwa na kwaya ya Bikira Maria ya Ubungo- Msewe wakati wa ibada sehemu ya kushukuru ukiwa na maneno yafuatayo:

> Mchanganyo mchanganyo bwana Yesu amekataa x4

> Kiburi kidogo unaweka kanisani nako umo humo,
> Dharau kidogo unaweka kanisani nako umo humo,
> Mchanganyo mchanganyo humo bwana Yesu amekataa.
>
> Uongo kidogo unaweka kanisani nako umo humo,
> Fitina kidogo unaweka kanisani nako umo humo,
> Mchanganyo mchanganyo humo bwana Yesu amekataa,
> Mchanganyo mchanganyo humo bwana Yesu amekataa.

Mabadiliko mengine yaliyoonekana katika nyimbo za ibada za Kikatoliki za sasa ni matumizi ya kejeli. Mathalani katika wimbo huu wa mchanganyo, mtunzi ametumia kejeli hasa alipoonesha mchanganyo wa tabia za watu katika kanisa, "kiburi kidogo unaweka, kanisani nako umo humo; dharau kidogo unaweka, kanisani nako umo humo" (Mstari wa 2 na wa 3). Aidha, mchanganyo wa "uongo kidogo na fitina kidogo" unaonekana kuondoa au kupunguza ukubwa wa kosa. Hivyo, tabia hiyo inahalalishwa na kukubaliwa kanisani kwamba si kosa, jambo ambalo si kweli kwa sababu kosa ni kosa tu hata lingekuwa dogo kiasi gani. Hivyo, tabia hiyo haitakiwi kanisani.

Kwa upande mwingine, mabadiliko ya utunzi wa nyimbo unaotokana na tafakuri ya mtunzi au maisha ya mtunzi yalionekana zaidi katika nyimbo za sasa za ibada za kikatoliki tofauti na nyimbo za zamani zilizotokana na Biblia, sala au tafakuri ya mababa watakatifu. Kwa ujumla, nyimbo za "Yesu Amechakachuliwa" na "Mchanganyo" zinatokana na tafakari au maisha ya watunzi. Mfano katika wimbo wa "Yesu Amechakachuliwa" mtunzi anamuona Yesu anayeabudiwa leo kanisani si yule Yesu wa miujiza, bali ni Yesu aliyechakachuliwa asiyekuwa na nguvu yeyote katika tafakuri yake. Aidha, katika wimbo wa "Mchanganyo" mtunzi anabainisha kuwa anayepaswa kwenda kanisani ni yule anayetenda matendo mema hasa ya kuepuka uongo, fitina, kiburi na dharau. Kamwe asiwe mtu wa kuchanganya kiburi na kanisa, dharau na kanisa (mstari wa 2 na 3) mambo ambayo hayatakiwi na Yesu.

Kwa kutumia wimbo huu, mtafiti pia aligundua kuwa melodia mchanganyiko za makabila ya Kitanzania kama ya Kihaya na Kihehe yametumika. Aidha, kutokana na nyimbo zilizochunguzwa, imebainika kuwa melodia za bongo fleva na taarabu sasa zinatumika katika nyimbo za ibada za kanisa Katoliki tofauti na nyimbo za zamani za Kilatini zilizojiegemeza kwenye utamaduni wa kigeni tu.

Aidha, kukua kwa sayansi na teknolojia nchini Tanzania na ulimwenguni kwa ujumla kumeleta mabadiliko makubwa katika nyimbo za ibada. Kupatikana na kuenea kwa "vifaa vilivyotumia umeme kama vile vinanda na magitaa", studio za kurekodia nyimbo, simu za mkononi, mitandao ya kijamii (Facebook, Youtube, Instagram na Twitter, n.k.) vimesaidia kuiweka dunia katika kijiji kimoja (Sanga, 2008:65). Hali hii imesababisha watu kuiga na kubadili tamaduni na mifumo yao ya maisha kwa haraka kwa malengo ya biashara na kwenda na wakati. Kanisa Katoliki

nalo halikubaki nyuma. Nyimbo nyingi zinazoimbwa ibadani zinatumia vifaa vya umeme kama vinanda, vipaza sauti na vinasa sauti. Pia, nyimbo nyingi za ibada zinarekodiwa na kuhifadhiwa katika mikanda ya video, CD, DVD na klipu zinazowekwa kwenye simu na mitandao ya kijamii na kuuzwa kwa watu ili kupata fedha za kujikimu kwa vikundi vya waimbaji wa nyimbo za ibada. Hali hii inasababisha waimbaji kuimba nyimbo za ibada zinazogusa jamii zaidi ili kupata soko.

Nadharia ya Utendaji inaeleza kuwa dhamira ya kazi ya kisanaa hutokana na jamii husika; na jamii huitathimini sanaa kwa kuijenga, kuiendeleza au kuirekebisha kadiri ya mahitaji yake (Mulokozi, 1996). Kutokana na nyimbo za ibada kuwa bidhaa inayohitajika na jamii, ilibainika kuwa dhamira za awali zilizolengwa na kanisa zilikosa nafasi katika soko badala yake dhamira za kijamii zilitawala. Mdau mmoja wa nyimbo za ibada na mwalimu wa kwaya, alidhihirisha hili aliposema kuwa, "nyimbo nyingi tunazoimba kanisani hivi sasa zina maudhui ya kijamii kama vile ndoa, mauaji ya vikongwe, albino, ugonjwa wa UKIMWI na UVIKO 19 ambazo hurekodiwa kwenye CD na DVD na kuuzwa." (Mahojiano, 25/11/2020). Aidha, dhamira zilizojitokeza katika nyimbo zilizochunguzwa ni zile zilizohusu jamii ingawa baadhi zilikuwa za kiroho kama ilivyokuwa awali (Kweka, 2013). Dhamira hizo ni: mauaji ya albino, vikongwe, ufisadi, UKIMWI, ujambazi, watoto yatima na wajane. Pia dhamira za upendo, umoja na ushirikiano katika jamii ziliendelezwa. Dhamira hizi zilibadilisha lengo la ibada na kulifanya kanisa kuwa chombo cha kuisemea jamii.

Kwa upande mwingine, mabadiliko ya dhamira ya nyimbo hizi yanaleta utata katika Kanisa Katoliki iwapo ndizo zinazopaswa kuimbwa kwenye ibada za Kikristo au la. Kwa ujumla, kazi ya sanaa haina mtazamo mmoja tu kwa kuwa sifa ya sanaa ambayo jamii moja ingeichukulia kuwa ni vigezo vya uzuri, katika jamii nyingine vingechukuliwa kama vigezo vya ubaya. Kutokana na majadiliano, waimbaji wa kwaya hizi walisema kuwa wana haki ya kuimba nyimbo zenye dhamira za mauaji ya albino, ufisadi, mauaji ya vikongwe, n.k. ili kuwaadilisha waumini na watu mbalimbali juu ya mwenendo mzuri wa kuishi kama Wakristo kwa sababu huo ndio upendo unaohubiriwa katika neno la Mungu. Aidha, uimbaji wa nyimbo zenye dhamira hizi kwa lugha za asili unatekeleza jukumu la utamadunisho katika kanisa. Utamadunisho katika muktadha wa Kanisa Katoliki ni hali ya kutumia nyimbo za asili, lugha ya asili na uchezaji ngoma za asili za wazawa katika kanisa. Hali hii hulifanya kanisa katoliki kuwa mahalia, yaani la wazawa wenye utamaduni fulani. Hata hivyo, uongozi wa kanisa umeona hali hii ni ya upotoshaji na isiyo na uchaji wa ibada. Padre Thomas Eriyo, mwenyekiti mstaafu wa Kamati ya Liturjia na Muziki Taifa, katika mahojiano juu ya nyimbo za ibada za Kikatoliki na dhana ya utamadunisho alibainisha hili:

> Dhana ya utamadunisho iliyotangazwa na Mtaguso wa Pili wa Vaticano na Papa Paulo VI, bado haijaeleweka vizuri miongoni mwa waimbaji na waumini. Watu wanafikiri kutamadunisha ni kuingiza katika kanisa kitu chochote wanachokitaka kama taarabu, bongo fleva na hata kutumia lugha zisizofaa katika ibada kama vile Yesu amechakachuliwa. (15/5/2020).

Kutokana na mawazo haya, ni dhahiri kuwa bado kuna utata miongoni mwa waumini na baadhi ya viongozi wa kanisa juu ya melodia zipi zitumike ibadani na zipi zisitumike. Aidha, mawazo haya yanataka uchambuzi wa makini wa lugha na maneno fulani tu yanayofaa kutumika kanisani, na yasiyofaa kutumika kama vile "Yesu amechakachuliwa". Kiuhalisia, kwa Kanisa Katoliki, Yesu hachakachuliwi. Padri Thomas Eriyo anasema "Yesu ni yule yule, jana, leo, kesho na hata milele; kamwe habadiliki wala kuchakachuliwa na mtu yeyote, na hiyo ndiyo imani na msimamo wa Kanisa Katoliki". Msigano wa dhana ya utamadunisho katika Kanisa Katoliki unawaweka baadhi ya viongozi wa kanisa katika nafasi ya kutokubali lugha inayotumika na kinachoimbwa wakati wa ibada. Wakati huo huo, wanakwaya wanaamini kuwa lugha wanayotumia na wanachokiimba ndicho kinachotakiwa katika ibada.

Naye Mangi (2022:5) anaona uimbaji wa kisasa unapotosha ibada kwa kuimba "nyimbo nyepesi nyepesi sana zenye teolojia finyu katika liturjia ya Kanisa Katoliki". Wepesi wa nyimbo hizi upo zaidi katika melodia na maneno yasiyokidhi teolojia ya Kikatoliki. Hata hivyo, uchaguzi wa lugha ipi itumike na kipi kiimbwe wakati wa ibada ni hoja tata kwani vigezo vitakavyotumika kuchagua lugha na melodia zinazofaa kuimbwa wakati wa ibada havijulikani. Lugha ni amali ya jamii inayotunza utamaduni, imani, mila na desturi za jamii kwa wakati husika (Schein, 2010:125). Hivyo, kanisa ni vema likatoa mwongozo unaofaa ili kuondoa utata huu kwani wote, waimbaji na viongozi wa kanisa, ni zao la jamii na wanajenga nyumba moja ya Mungu. Hivyo, ushirikiano, umoja na upendo kati ya waimbaji, waumini na viongozi wa ibada ni muhimu sana katika kujenga Kanisa Katoliki, utamaduni na taifa la Tanzania kwa ujumla.

Kutokana na utandawazi, uchunguzi ulibaini kuwa uimbaji wa nyimbo za ibada sasa umekuwa biashara inayotafsiriwa kwa vigezo vya jicho la uzuri na ubora ambavyo hujengwa na tamaduni za jamii za wakati husika. Ili biashara ifanyike, waimbaji wa nyimbo hizi walivaa mavazi yaliyoboresha uimbaji wao kadiri ya jamii ilivyopenda na siyo kulingana na ibada. Wengine walibuni mitindo mipya ya mavazi au waliiga mavazi kutoka sehemu mbalimbali ilimradi tu wavutie biashara ya nyimbo zao (Wagner, 2019). Kwa mfano, katika kwaya zote mbili zilizotafitiwa, waimbaji wake wote, wa kike na wa kiume, walionekana kuvaa suti nzuri tofauti na kipindi cha nyuma walipovaa majoho. Mwalimu wa kwaya ya Ubungo-Msewe alipohojiwa juu ya kuvaa suti badala ya majoho alisema, "kuvaa suti kunapendezesha kwaya na waimbaji wote huonekana watanashati na hivyo kwenda

na wakati" (Mahojiano, 20/3/2020). Hata hivyo, utafiti ulibaini kuwa baadhi ya suti zilizovaliwa na wanakwaya zimebana sana kiasi cha kuonesha maumbo yao.
Aidha, mdau mwingine wa muziki wa Kanisa Katoliki alipoulizwa jinsi anavyowaona waimbaji wakati wa ibada alisema, "waimbaji wetu wamekuwa wakiiga uvaaji usiostahili kama nguo fupi zilizobana na kuonesha maungo yao hasa wakina dada. Waimbaji wa kiume wengine huvaa mlegezo mambo ambayo hayatakiwi wakati wa ibada kwa sababu huwakwaza watu" (Mahojiano, 20/2/2020, Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu). Uvaaji wa namna hii unaondoa uchaji wa mtu katika ibada na badala yake kumpa mihemko inayovuruga na kuondoa moyo wa unyenyekevu na toba. Hivyo, waimbaji yafaa wavae nguo zinazostahili hasa zisizobana wala kuonesha maungo ya mwili ili kuleta uchaji wa ibada.

Kutokana na majadiliano na wanakwaya, utafiti uligundua kuwa waimbaji wa sasa wa Kanisa Katoliki wanapenda kuimba na kucheza. Uchezaji wao wameiga kutoka kwa waimbaji wa muziki wa Injili, Bongo Fleva, ngoma za kiasili na muziki wa Kongo hasa Rumba. Waimbaji walichanganya mitindo mbalimbali ya uchezaji kadiri ya nyimbo zilivyotumika katika ibada. Baadhi ya nyimbo walizoimba na kucheza wakiwa wamesimama na nyingine wakiwa wameketi, hasa wimbo wa mwanzo wa sadaka na nyimbo za komunyo. Wimbo ulipowavutia waumini nao walishiriki "kuimba, kucheza, kupiga vigelegele, miluzi na hata kushangilia" (Mkallyah, 2016:315). Kwa mfano, Jumapili ya tarehe 9/2/2020, mtafiti alishuhudia wanakwaya wa Ubungo-Msewe wakiimba na kucheza kwa mitindo mchanganyiko, mara wakizungusha mwili na kuinama na baadaye kuinuka huku mikono yao ikiwa chini, mara wakitembea na kunesa wakiinua mikono juu huku wakipiga makofi yakichagizwa na vigelegele. Uchezaji huu ulibadili hali ya ibada kutoka utulivu na uchaji, kuwa ya shangwe na uchangamfu, jambo ambalo halikuwepo katika ibada za Kikatoliki. Uchezaji huu kwa baadhi ya waumini na viongozi wa kanisa ni kikwazo. Mangi (2022:5) anasema, "wanakwaya wakicheza sana hufisha moyo wa sala na kuzingatia zaidi burudani." Kwa hoja hii, kuimba na kucheza ni kuharibu sala, na kuimba bila kucheza ni kusali. Hivyo, yafaa wanakwaya wanapoimba nyimbo za ibada watulie ili kupata uchaji wa sala.

Kwa upande wa waimbaji, utafiti uligundua kuwa uchezaji uliwafanya wafurahi na waonekane zaidi na watu wengi kanisani. Aidha, waimbaji waliocheza kwa madaha wakiwa na sare zao waliwavutia na kuwafurahisha waumini na hivyo, walipewa zawadi hasa pesa. Mwimbaji wa zamani wa kwaya ya Mtakatifu Paulo Ubungo-Msewe alipoulizwa juu ya athari ya uchezaji wakati wa ibada alisema; "waimbaji wanapoimba na kucheza katika ibada huwafanya waumini wafurahi, hata kama mtu alikuwa na huzuni hutoweka na kurudi nyumbani akiwa na furaha na matumaini mapya katika maisha yake" (Mahojiano, 15/1/2020). Hivyo, uchezaji wakati wa kuimba nyimbo za ibada uliwafanya waimbaji na waumini kufurahi na kupenda ibada yao. Aidha, uimbaji wa melodia za Kiafrika ukiambatana na kucheza wakati wa ibada za Kikristo ndio utamaduni wa Kiafrika unaowapa uhuru Waafrika wa

kujenga na kuendeleza kanisa la Mungu kwa misingi ya Kiafrika katika ardhi yao (Mbunga, 1968; Mbiti, 1968).

Katika kuchunguza muktadha, hali ya uimbaji katika Nadharia ya Utendaji huathiriwa na uhusiano uliopo kati ya "mwimbaji na eneo halisi au lisilo halisi linalotumika kuimbia" (Mulokozi, 1996:18). Uhusiano huu unaonekana katika eneo la kuimbia lilivyosaidia kukuza na kuboresha uimbaji. Kutokana na data zilizokusanywa, utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za ibada zilizoimbwa tangu wakati wa uhuru hadi miaka ya 1990 zilitumika makanisani tu na si mahali pengine. Nyimbo hizi zilijenga na kulinda muktadha wa Kanisa Katoliki. Mdau mwingine wa mziki na kiongozi wa Kanisa Katoliki Ubungo Msewe alithibitisha hili aliposema, "uimbaji wa nyimbo za ibada za Kikatoliki ulikuwa wa kanisani tu, lakini hivi sasa nyimbo hizi zinaimbwa hata kwenye vyombo vya usafiri na katika sherehe mbalimbali" (Mahojiano, 13/4/2019). Kutokana na muktadha huo, nyimbo za ibada kwa kipindi cha nyuma ziliheshimiwa na kutumika kama sala na njia mojawapo ya kukuza uchaji wa Mungu.

Kipindi hiki, muktadha wa matumizi ya nyimbo za ibada za Kikatoliki hivi sasa umepanuka zaidi. Kwa mfano, mtafiti alishuhudia waimbaji wa kwaya ya Bikira Maria Ubungo Msewe wakiimba wimbo wa "Enyi Watu Wote Pigeni Makofi" kwenye ukumbi wa sherehe ya mahafali ya mwanachuo mmoja hapo Ubungo. Wanakwaya waliimba wimbo huu huku wakicheza na kupiga makofi pamoja na hadhira ambao wengine walikuwa Waislamu, Wapentekoste na wale wenye dini za asili.

Pia, utafiti huu ulibaini kuwa tangu miaka ya 1990 hadi sasa nyimbo za ibada ziliimbwa na kurekodiwa katika mazingira mbalimbali yasiyokuwa ya ibada kama vile mlimani, kwenye mto au bahari na kwenye mbuga za wanyama na kurushwa katika vituo vya televisheni, redio na mitandao ya kijamii. Pia, mtafiti alishuhudia baadhi ya nyimbo za ibada zikichezwa katika televisheni na redio, kwenye kumbi za starehe, viwanja vya michezo, magari ya matangazo na katika sherehe zisizo za kidini. Hivyo, ujumbe wa nyimbo hizo huwafikia watu wengi zaidi ya wale wanaohudhuria kanisani na wasio wa imani hiyo. Hali hii inakuza "umoja, ushirikiano na upendo miongoni mwao" hususani Watanzania, bila kujali itikadi za dini zao, bali kufanikisha kile kilichowakutanisha (Adeola, 2020:92). Hali hii ilikoleza imani ya Kikristo iliyosababisha nyimbo hizi kutumika sehemu mbalimbali hata za starehe. Aidha, matumizi ya nyimbo za ibada katika shughuli za starehe yameongeza wigo wa matumizi ya nyimbo hizi.

## 6.0 Mambo Yaliyosababisha Mabadiliko ya Kiuimbaji katika Kanisa Katoliki

Kutokana na data zilizokusanywa, uimbaji wa nyimbo za ibada za Kikatoliki Tanzania kwa lugha ya Kilatini na Kiingereza ulianza kupungua kuanzia miaka ya 1970. Jambo hili lilitokana na mwamko wa Watanzania kuthamini na kutumia

utamaduni wao katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiulinzi na kiutamaduni ulioanzishwa wakati wa uhuru. Mwimbaji wa nyimbo za Kilatini katika Kanisa kuu la Mtakatifu Yosefu alipohojiwa chanzo cha mabadiliko ya nyimbo katika kanisa alisema, "kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 kulichochea matumizi ya nyimbo za Kiswahili kutumika sehemu zote hata kanisani" (Mahojiano, 2/2/2017). Matumizi ya Kiswahili yalitokana na mawazo ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Tanganyika na baadaye mwaka 1964 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kufufua na kutumia utamaduni wa Mtanzania uliodhoofishwa na wakoloni. Ngoma, nyimbo za asili na lugha ya Kiswahili vilisisitizwa sana katika taasisi zote za elimu, dini, afya na serikali kwa ujumla.

Vilevile, kuanzishwa kwa Wizara ya Utamaduni mwaka 1962 kuliongeza nguvu ya kutekeleza jukumu hilo. Vikundi mbalimbali vya sanaa vikiwamo Paukwa, DDC Kibisa na vinginevyo vilianzishwa (Songoyi, 1988). Aidha, nyimbo za kigeni kama *Pater Noster* -Baba yetu, *Agnus Dei* – Mwanakondoo, n.k, zilizotumika katika ibada za Kikristo zilitafsiriwa kwa Kiswahili na lugha nyingine za asili za Kitanzania kama vile Kisukuma, Kinyakyusa, Kinyamwezi na Kihaya, na zilitumika katika ibada za Kikristo (Odwar, 2005; Emielu, 2014). Mabadiliko haya yaliwafanya Watanzania kujiona wako kwenye ardhi ya nchi yao kwa kutumia na kukuza utamaduni wao.

Mtaguso wa II wa Vatican uliosisitiza ibada za Kikatoliki ziendeshwe kwa lugha mahalia za kila taifa ulisababisha mabadiliko ya uimbaji katika nyimbo za ibada za Kikatoliki (Mbunga, 1963; Flannery, 1975). Hali hii iliongeza chachu kwa Watanzania wengi kuipenda dini ya Kikristo kwa kujifunza neno la Mungu kwa lugha ya Kiswahili, hivyo, kusaidia kanisa kukua kwa haraka. Aidha, Sinodi ya Afrika ya 1987 ilikazia zaidi matumizi ya lugha mahalia za kila jamii (Paul, 1995). Watu walisali na kuimba nyimbo za ibada hata kwa lugha zao za asili, hivyo, ujumbe uliohubiriwa kanisani uliwafikia waumini kwa haraka. Pia, kwa kuimba nyimbo za kiasili kanisani, watu wengi waliotengwa na Wamisionari kama wenye dhambi na wapagani sasa waliruhusiwa kanisani. Hali hii iliwavutia watu wengi kujiunga na kanisa kwa kubatizwa na kuwa wafuasi wa Mungu (Mkallyah, 2016).

Nadharia ya Utendaji hujielekeza katika sanaa inayoleta mabadiliko katika jamii. Uimbaji wa nyimbo kwa lugha mahalia ulitawala ibada za Kikatoliki na kusababisha uimbaji wa kuongozwa na padre au katekista kubadilika. Vikundi vya waumini wachache vilivyoitwa 'kwaya' vilianzishwa (Barz, 2003 na Collins, 2014). Kwaya hizi ziliimba nyimbo zilizoongoza ibada na zilichochea matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha za asili ya Tanzania (Mkallyah, 2016; Kidula, 2008). Pia, vikundi hivi vilibadili fikra za Watanzania kwa kuthamini utamaduni wa Mtanzania katika nyanja zote na kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa wananchi, kanisa na taifa zima.

Kwa upande mwingine, utafiti huu ulibaini kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopatikana miaka ya 2000 hadi sasa, hasa televisheni, simu janja, vishikwambi na mitandao ya kijamii kama *Youtube*, *Facebook*, *X* (zamani, *Twitter*) na *Instagram* yaliiweka Tanzania na dunia katika kijiji kimoja chenye tamaduni mbalimbali zinazopatikana kwa wakati mmoja kwa haraka na kwa watu wengi. Melodia mbalimbali za kiasili zilizopatikana katika mitandao ya kijamii ziliwapa urahisi walimu wa kwaya kutumia melodia hizo katika nyimbo za ibada. Mwalimu wa kwaya ya Bikira Maria Ubungo Msewe anasema, "baadhi ya nyimbo za asili za ibada nilizichukuwa kutoka kwenye mitandao" (Mahojiano, 22/2/2021). Hivyo, kwa kutumia mitandao, melodia nyingi za asili ziliingizwa kanisani na kutumika pasipo kuwa na mpaka. Kwa mfano, melodia za Kihaya, Kihehe, Kisukuma na Kifipa zilizochunguzwa katika utafiti huu, zilibainika kuchukuliwa katika jamii hizo na kuwekewa maneno kutoka katika Biblia. Nyimbo hizi zinaendelea kutumika hadi sasa katika ibada. Aidha, kutokana na utandawazi, nyimbo hizi zilirekodiwa na kuhifadhiwa katika mikanda ambayo ilichezwa sehemu mbalimbali; hivyo, watu wengi waliziona na kuzitumia nyimbo hizo katika shughuli zao. Mikanda hii ilisaidia sana kusambaza na kueneza melodia za kiasili katika sehemu nyingi hasa katika ibada za Kikristo.

## 7.0 Hitimisho

Makala haya yamebainisha mabadiliko ya kiuimbaji katika nyimbo za ibada za Kikatoliki. Mabadiliko haya yalionekana hasa katika eneo la kuimbia, matumizi ya lugha, maudhui, melodia, waimbaji, uchezaji, vifaa vya muziki, na nyimbo kuwa bidhaa inayouzwa na kuinua uchumi wa mtu mmoja, kwaya na kanisa kwa ujumla. Hapo awali nyimbo za ibada za Kikatoliki nchini Tanzania zilitumia lugha za Kilatini na Kiingereza. Aidha, katika makala haya imebainishwa kuwa hivi sasa lugha ya Kiswahili na lugha za kiasili za makabila ya Kitanzania zinatumika katika nyimbo za ibada. Kejeli, lugha za mitaani na melodia za makabila ya Kitanzania, Kikongo na hata Bongo Fleva zilibainika kutumika katika nyimbo za ibada. Aidha, maudhui ya nyimbo yamebadilika kutoka kuomba toba, kunyenyekea na kutafakari ukuu wa Mungu tu, hadi kuelezea mauaji ya albino, mauaji ya vikongwe, ubakaji, na ugonjwa wa UKIMWI.

Nadharia ya Utendaji ilitumika kuchunguza jinsi wanakwaya wanavyoimba wakati wa ibada. Kutokana na uchunguzi huo, makala yamebainisha kuwa waimbaji wametawaliwa na uchezaji wa mitindo mbalimbali bila kuzingatia muktadha unaowataka kuimba wakiwa wametulia ili kutafakari mafumbo matakatifu ya Mwili na Damu ya Yesu Kristo. Hali hii kwa historia ya uimbaji katika kanisa Katoliki ni mapokeo tu yasiyojali uchaji katika ibada.

Aidha, imebainishwa kuwa mandhari ya waimbaji wa nyimbo za Kikatoliki imepanuka sana. Nyimbo za ibada hivi sasa haziimbwi kanisani tu, bali hata katika viwanja vya michezo, kumbi za starehe vyombo vya usafiri na vyombo vya habari

kama redio na televisheni. Kwa upande mwingine, kwaya zote zilizochunguzwa zilitumia vifaa mchanganyiko, kinanda cha umeme, njuga, filimbi, kayamba na ngoma. Matumizi ya ala, melodia na lugha za kiasili kanisani yaliwafanya Watanzania kujisikia huru na kuona kanisa ni la kwao.

## Marejeleo


Adeola, T. S. (2020) “Gospeltainment: Music and Profit in Nigeria”. *Utafiti*, Juz. 15(1): 81-100.

Barz, G. (2003) *Performing Religion: Negotiating Post and Present in Kwaya Music of Tanzania*. Amsterdam: Rodopi.

Baur, J. (2005) *2000 Years of Christianity in Africa*. *An African Church History*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (2007) *Muundo wa Misa: (Umuhimu wa Kuimba).* Ndanda: Benedictine Publications.

Blackwell, P. (2004) “Literary Realism". Inapatikana katika https://onlinelibrary.wiley.com.doi/book/10.1002/978047075664. Ilisomwa tarehe 20 Mei 2021.

Chitanda, E. (2002) *Singing Culture: A Study of Gospel Music in Zimbabwe*. Uppsala: Nordiskainstitutent.

Collins, E. J. (2004) “Ghanaian Christianity and Popular Entertainment: Full Circle”. *History in Africa*, Juz.31: 407 – 423.

Collins, E. J. (2014) “The Ghanaian and Nigerian Gospel Music Explosion.” *Journal of Performing Arts*, Juz. 4.(4):115 – 132.

DeBellis, M. (1995). *Music and Conceptualization*. Cambridge: Cambridge University Press.

Emielu, A. (2010) “Music and Pentecostalism in Nigeria: The Afro-American Influence”. Katika S. O. Oyewole, A. P. Dopamu, I. O. Umejesi, P. O. Amanze, V. A. Alabi na S. E. Ododo (Wah.) *Science in the Perspective of African Religion (AFREL), Islam and Christianity*. Ilorin: Nastrens. Kur. 287-298.

Emielu, A. (2014) “I am a Music Minister, not a Musician: Social Identity in Contemporary African Music”. *Nigerian Music Review*, Juz. 13: 110 – 126.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa*. Oxford: Oxford University Press.

Flannery, A. (1975) *Mtaguso wa II wa Vatikani*. Roma: St. Paul Publications.

Kaombe, S. (2013) *Pamoja Tumsifu Mungu: Kitabu cha Nyimbo*. Dar es Salaam: Nesmap Print Technology.

Kidula, J. (2013) *Music in Kenyan Christianity*. Bloomington: Indiana University Press.

Kidula, J. (2008) *Music Culture African Life, in Music in The Life of African Church*. New York: Baylor University Press.

Kilaini, M. (2005) *Kitabu cha Nyimbo Kumbukumbu ya Kardinali Rugambwa. Jimbo Kuu la Dar es Salaam*. Morogoro: Clarentian Publications.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. (2005) *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kivy, P. (2001) *Introduction to Philosophy of Music*. Oxford: Clarendon Press.

Kweka, N. (2013) *Uchambuzi wa Dhamira katika Nyimbo za Muziki wa Injili Dar es Salaam*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Lihamba, A. (2004) "Tanzanian Theatre". Katika M. Banham (Mh.) *A History of African Theatre*. Cambridge: Cambridge University Press. kur. 223 – 247.

Mangi, P. (2015) "Wanakwaya Hawapaswi Kuimba Nyimbo Zisizojulikana kwa Waumini". *Kiongozi*. 21 Mei 2015. uk.18.

Makoye, H. (1996) *Tanzanian Traditional Dances:* Choreography *and Communication in Urban Dar es Salaam.* Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Malema, L. (1990) *Nyimbo za Kikwetu*. Tabora: TMP Print**.**

Mbunga, S. (1963) *Church Law and Bantu Music*. Switzerland: Nouvelle Revue de Science Missionnare Suisse.

Mbunga, S. (1968) "Music Reform in Tanzania". *Africa Ecclesiastical Review*, Juz.1: .23-47.

Mbiti, J. (1968) *African Religions and Philosophy*. New York: United States of America.

Mulokozi, M. M. (1996) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: OUT.

Mkallyah, K. (2016) "Affect and Effect of Indigenous Tanzanian Music Tradition in Christian Church Worship in Tanzania". *Ethnomusicology*, Juz.60 (2):300 – 328.

Mkallyah, K. (2005) *The Emergence and Use of African Theatre in Church Choir Performance*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Odwar, H. (2005) *Music Education in Kenya*. *A Historical Perspective*. Eldoret: Kijabe Printing Press.

Paul, J. (1995) *Post- Synodal Apostolic Exhortation. The Church in Africa*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Sanga, I. (2010) "The Practice and Politics of Hybrid Soundscape in Muziki wa Injili in Dar es Salaam, Tanzania". *Journal of African Cultural Studies*. Juz. 22(2):145 – 156.

Sanga, I. (2008) "Music and Nationalism in Tanzania: Dynamics of National Space in Muziki wa Injili Dar es Salaam". *Ethnomusicology*, Juz. 52 (1):52 – 84.

Sanga, I. (2006) "Composition Processes in Popular Church Music in Dar es Salaam Tanzania". *Ethnomusicology Forum*, Juz.15 (2): 247 – 271.

Songoyi, E. (1988) *Commercialization. Its Impact on Traditional Dances*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Schein, E. (2010) *Organizational Culture and Leadership.* Fourth Edition. San Francisco: CA Press.

Schwartz L.Y. (2010) *Nadharia ya utendaji wa Jumla*. Oxford: Elimu ya Juu Press

TUKI. (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wagner, T. (2019) *Music, Branding and Consumer Culture in Church*: *Hillsong in Focus*. London: University of London.

Wagner, T. (2016) *Christian Congregational Music: Performance, Identity and Experience*. London: Palgrave McMillian.

Wamitila, K.W. (2004) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher Ltd.

Yung, B. (2019) *Exploring Creativity in Traditional Music*: *Yearbook for Traditional Music.* Cambridge: Cambridge University Press.